# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Desemba 2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022**



## SALAM KUTOKA KWA MKURUGENZI



***Bw.Jimson Mhagama-Mkurugenzi Mtendaji-Same***

## *Wanafunzi wote waliofaulu waripoti shuleni,na wenye umri wa kuanza shule wote waandikishwe*

*Nawatakia heri ya Mwaka Mpya 2025 Wananchi wote wa Wilaya ya Same. Mwaka 2024 umemalizika salama na ninashukuru kwa ushirikiano mkubwa mlioutoa kwa Serikali katika kuhakikisha kuwa masuala mbalimbali ya maendeleo yanasonga mbele.*

*Msimu wa sherehe mbalimbali za mwisho wa mwaka tumeumaliza, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha tena kwenye ujenzi wa Taifa letu la Tanzania.*

*Napenda kuwakumbusha ndugu zangu wa Wilaya ya Same kwamba jukumu kubwa liliopo mbele yetu kwa sasa ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wanaripoti shuleni bila kukosa.*

*Kwenye Wilaya yetu ya Same Jumla ya wanafunzi 6,151 walimaliza darasa la saba mwaka jana na kati yao asilimia 73 walifaulu na wamechaguliwa kujiunga na Sekondari, kwahiyo*

*wanafunzi wote waliochaguliwa tunataka kuwaona shuleni.*

*Kwa kutambua kuwa elimu ni msingi bora wa maisha ya mtoto tayari wilaya inayo shule na madarasa ya kutosha kupokea wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Sekondari.*

*Tukumbuke kuwa Serikali inatekeleza Sera ya Elimu bure ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata fursa ya kupata elimu bila kuwa na kisingizio chochote, hivyo hakuna sababu ya mzazi kutompeleka mtoto shule.*

*Niwakumbushe pia wazazi wenye watoto wenye umri wa kuanzia miaka mitano kuhakikisha kuwa wanawaandikisha darasa la awali na darasa la kwanza, uandikishaji umeanza mwezi Desemba 2024 na utakamilika Machi 31, 2025.*

*Serikali imetoa muda wa kutosha kwa wazazi kuhakikisha kuwa wanawaandikisha kuanza darasa lwa kwanza watoto wote wenye umri wa kwenda shule, wazazi mtambue kuwa ni kosa kutompeleka mtoto shule.*

*Kila mtoto ana haki ya kupata elimu hivyo kila mzazi atimize wajibu wake wa kuhakikisha kuwa anampeleka mtoto shule na pia kuhakikisha anafuatilia maendeleo ya mtoto wake shuleni.*

*Mwaka huu tunatarajia kuandikisha wanafunzi 5,518 darasa la awali na wanafunzi 5,672 darasa la kwanza na hadi kufikia Januari 10, 2025 kwa darasa la kwanza tumefikia asilimia 79 ya uandikishaji na darasa la awali tumefikia asilimia 75, tunahitaji kufikia asilimia 100 ifikapo Januari 31,2025 .*

*Elimu ni ufunguo wa maisha, hakikisha unampatia mwanao ufunguo.*

# HERI YA MWAKA MPYA 2025

# MKANDARASI WA MRADI WA MAJI KIHURIO ATAKIWA KUKAMILISHA MRADI KWA WAKATI



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni (katikati ) akishuhudia utiaji saini wa Mkataba wa Mradi wa Maji Kihurio wenye thamani ya shilingi Bil.4.1.***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni ameitaka kampuni ya Fesam Construction Limited iliyosaini Mkataba wa kutekeleza Mradi wa Maji Kata ya Kihurio kuhakikisha utekelezaji wa mradi unafanyika kwa viwango na unakamilika kwa wakati ili kuondoa kero ya ukosefu wa Maji kwa wananchi wa Kata hiyo.

Mkuu wa Wilaya ametoa agizo hilo katika hafla fupi ya utiaji Saini Mkataba wa kutekeleza Mradi huo wenye thamani ya shilingi bilioni 4.17.

Mheshimiwa Kasilda pia amewataka wananchi wa Kihurio kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa Mkandarasi kwenye kipindi chote cha utekelezaji wa mradi, ikiwa ni pamoja na kila mmoja kuwa mlinzi wa kwanza wa mitambo itakayotumiwa na wakandarasi kutekeleza mradi huo.

“Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendeleza jitihada zake za dhati za kumtua mama ndoo kichwani" Alisema Kasilda.

Alisema mradi huo unaenda kuwa mkombozi kwa Wananchi wa Kihurio ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakiteseka na kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji kwenye mito.

Akitoa taarifa ya Mradi huo Meneja wa Wakala wa maji safi na usafi wa mazingira Vijijini (RUWASA) Mhandisi Abdallah Gendaeka amesema, mradi utatekelezwa kwa muda wa miaka miwili kuanzia Desemba 06 mwaka huu na kutarajiwa kukamilika Desemba 06 mwaka 2026.

Alisema kuwa kazi hiyo itafanywa na mkandarasi kutoka kampuni ya FESAM CONSTRUCTION LIMITED yenye makao makuu yake Jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake, Meneja wa Ruwasa mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Weransari Munisi, alisema kuwa kupatikana kwa fedha za mradi huo kunachagizwa na jitihada za Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki Anne Kilango kwa lengo la kutaka Wananchi wake kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Fesam Construction Limited, Mhandisi Charles Maganga, ameahidi kuifanya kazi hiyo kwa wakati kulingana na mkataba unavyomtaka ili mradi uweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Pili Salim, Mkazi wa Kata hiyo alisema kukamilika kwa mradi huo kutakuwa suluhisho juu ya adha wanayoipata ya kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji kwenye mito.

# LIPA KODI YA PANGO LA ARDHI KWA WAKATI

# DAS SAME AONGOZA KUFANYA USAFI MAADHIMISHO YA UHURU DESEMBA 9



***Katibu Tawala wa Wilaya ya Same Bi. Upendo Wella (kushoto) akishirikiana na wananchi kufanya Usafi kwenye eneo linalozunguka Hospitali ya Mji Same kama sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Uhuru Desemba 9.***

Katibu Tawala wa Wilaya ya Same Bi.Upendo Wella leo ameongoza mamia ya Wananchi wa Same kufanya usafi na kuotesha miti kwenye chanzo cha Maji cha Water kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Akizungumza baada ya kukamilika kwa zoezi hilo Katibu Tawala Bi. Wella aliwataka wananchi kujenga tabia ya kufanya usafi kwenye maeneo yote yanayowazunguka.

"Leo tumeadhimisha siku ya Uhuru Kwa kufanya usafi na kuotesha miti hivyo shughuli hizi ziwe endelevu" alisema

Aidha aliwataka wananchi kuendelea kulinda na kudumisha amani ambayo imeendelea kuwepo kwa miaka 63.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama aliwashukuru wananchi kujitokeza kwa wingi kuadhimisha siku ya Uhuru.

"Mwitikio umekua mkubwa,wananchi wamejitokeza kwa wingi kufanya usafi na tumeotesha miti zaidi ya 100 kwenye chanzo cha Maji cha Water "alisema Bw.Mhagama.

## VIJANA ,WANAWAKE NA WENYE ULEMAVU WASHAURIWA KUOMBA MIKOPO YA 10%



***Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same Bw.Charles Anatoly akitoa mafunzo kwa maafisa Maendeleo ya Jamii juu ya namna ya kuomba mkopo kupitia Mfumo ili waweze kuwaelekeza Wananchi.***

Kufuatia kufunguliwa kwa dirisha la mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Wilaya ya Same imetoa mafunzo kwa maafisa Maendeleo ya Jamii  zaidi ya 30 ngazi ya Kata juu ya utaratibu wa kuwasilisha maombi kupitia mfumo wa Wezesha Portal.

Akitoa mafunzo kwa maafisa hao Afisa Maendeleo Wilaya ya Same Bw. Charles Anatoly alisema kwasasa mfumo wa unaotumika kupokea maombi ni mfumo ulioboreshwa ambao unawezesha mchakato wa upatikanaji wa mkopo kwa haraka.

Alisema Mfumo huo ujulikanao kama Wezesha Portal umeshafanyiwa majaribio na umeonesha mafanikio hivyo maafisa Maendeleo Kata wamepewa elimu ili waweze kuwasaidia wanavikundi kuomba mkopo kwenye mfumo.

”Serikali imeboresha mfumo wa uombaji wa mikopo ili kuviwezesha Vikundi kuomba mikopo kwa urahisi na kuharakisha mchakato wa wao kupata mikopo”alisema Bw.Anatoly

Maombi ya mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu yameanza kupokelewa kupitia mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz na mwisho wa kupokea maombi ni Oktoba 10,2024.

Halamshauri ya Wilaya ya Same ina vikundi zaidi ya 100 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vimesajiliwa na vina sifa ya kuomba mikopo hiyo.

“Mikopo ya awamu hii itatolewa kwa vikundi ambavyo havidaiwi na halmashauri,kama kikundi kinajua kina deni la nyuma kilipe kwanza deni ndio kiombe mkopo mwingine”alisema Bw. Anatoly

## WANANCHI WATAKIWA KUENDELEZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI




***Mabango mbalimbali yenye ujumbe wa mapambano dhidi ya UKIMWI yakionyeshwa kwa wananchi kwenye maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani Desemba 1, 2024.***

Wananchi wa Wilaya ya Same wametakiwa kujitokeza kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya na ushauri nasaha kwaajili ya kupima afya zao na kupata ushauri juu ya kujiepusha na ugonjwa hatari wa UKIMWI.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni wakati akizungumza na wananchi wa Same kwenye maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani ambayo hufanyika Desemba Mosi ya kila mwaka.

Lengo la maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani ni kuwakumbuka watu waliopoteza maisha kutokana na ugonjwa wa UKIMWI lakini kukumbushana njia sahihi za kuzingatia ili kuepuka maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Shughuli za maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani pia huenda sambamba na kukumbushana umuhimu wa kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI (ARV’s) kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Akizungumza na Wananchi kwenye uwanja wa kwasakwasa mjini Same Mkuu wa Wilaya aliwahimiza wananchi kwenda kupima afya zao ili kujua hali zao na waweze kuchukua hatua stahili kulingana na majibu watakayoyapata.

“Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali ya Dkt Samia Suluhu Hassan inaendelea kuboresha huduma za afya ikiwemo kuhakikisha upatikanaji wa dawa za ARV’s kwa watu wote wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Katika Maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani Mkuu wa Wilaya ya Same pia alizindua Kampeni ya Mwezi wa Afya na Lishe kwa roundi ya Desemba itakayofanyika kuanzia tarehe 1-30 Desemba katika vituo vyote vya huduma za Afya Wilayani Same.

Maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani  yalikwenda sambamba na shughuli mbali mbali za lishe ikiwemo upimaji wa hali ya Lishe(Uzito, Urefu (BMI), MUAC kwa watoto chini ya miaka mitano, utoaji wa matone ya Vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto wa chini ya miaka mitano.

Shunguli nyingine zilizofanyika ni maonyesho ya mapishi bora na utengenezajji wa juice na mapishi ya mbogamboga  na matumizi ya viungo va vikolezo(Herbs and spices) ambavyo ni muhimu kiafya.

Siku ya UKIMWI Duniani kwa mwaka huu imebebwa na kaulimbiu isemayo Chagua njia sahihi,Tokomeza UKIMWI.

# KULENI MLO KAMILI KULINDA AFYA ZENU-DED SAME



***Makundi mbalimbali ya vyakula yaliyoonyeshwa kwenye hafla ya siku ya Lishe Wilayani Same iliyofanyika kwenye Kata ya Ruvu.***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama amewashauri wananchi kuhakikisha kuwa wanakula mlo kamili ili kulilinda afya zao dhidi ya magonjwa mbalimbali.

Alitoa ushauri huo wakati wa maadhimisho ya siku ya lishe yaliyofanyika kwenye Kata ya Ruvu Wilayani hapa.

Mkurugenzi huyo alisema kuna haja kubwa kwa wananchi kuzingatia ushauri wa wataalam wa lishe kwenye ulaji ili kuwa na afya bora,hasa kwa kinamama wajawazito na watoto.

"Wataalam wanatwambia tukila mlo kamili miili yetu inajenga kinga Imara hivyo inakuwa sio rahisi kushambuliwa na maradhi"alisema Bw.Mhagama.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake wa Hospitali ya Wilaya Same Dkt.Steven Temanyika alisisitiza kula mlo kamili kwa kinamama wajawazito na watoto.

Alisema wajawazito wanapokosa mlo kamili afya yao na ya mtoto aliye tumboni huathirika kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kuishiwa damu.

"Kwenye nchi zilizoendelea tatizo la upungufu wa damu kwa wajawazito ni asilimia 10 hadi 20 wakati kwenye nchi zatu zinazoendelea ni asilimia 40 hadi 80"alisema Dkt.Temanyika

Akitoa elimu ya lishe kwa wananchi Afisa Lishe wa Wilaya ya Same Bi.Jackline Kilenga alisema ni vyema kila mtu ahakikishe kuwa kwenye mlo wake kuna wanga,vitamin na protini.

## TUMIENI MAJI TIRIRIKA KUNAWA MIKONO MARA KWA MARA-AFISA AFYA.



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama akionyesha njia sahihi ya kunawa mikono kwa maji tiririka, aliyesimama kulia ni Afisa Afya wa Wilaya ya Same Bi.Yuster Malisa, wengine ni wananchi waliohudhuria hafla fupi ya siku ya lishe kiwilaya.*

Wananchi wa Wilaya ya Same wametakiwa kuwa na vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka majumbani kwao na kwenye biashara zao ili kujilinda na magonjwa ya mlipuko.

Wito huo umetolewa na Afisa Afya wa Wilaya ya Same Bi.Yuster Malisa wakati wa maadhimisho ya siku ya lishe Wilayani Same.

"Suala la kunawa mikono kwa maji tiririka ni muhimu kwa Afya ya kila mmoja wetu,hivyo ni vyema kila familia na wafanyabiashara kuweka kifaa cha kunawia mikono kwa maji tiririka "alisema Yuster.

Abasi Mshana ni mfanyabiashara wa chakula Wilayani Same ambaye anasema wananchi wengi kwasasa wanaelewa umuhimu wa kunawa mikono.

"Yangu ugonjwa wa Corona utusumbue wananchi wamekua Sana umuhimu wa kunawa mikono maana hata maji yakiisha ukichelewa kujazia wanakufuata kuhitaji maji"alisema.

## MANUNUZI YOTE YA UMMA YAFANYIKE KWENYE MFUMO WA NesT-PPRA



***Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma Kanda ya Kaskazini Bw.Magai Maregesi (wa kwanza kushoto) akizungumza na wajumbe wa CMT Halmashauri ya Same.***

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa manunuzi ya Umma (PPRA) Kanda ya Kaskazini Bw.Magai Maregesi amekumbusha umuhimu wa kuhakikisha kuwa manunuzi yote ya Umma yanafanyika kupitia mfumo wa NesT.

Ameyasema hayo wakati akizungumza na Timu ya Menejimenti (CMT) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same wakati wajumbe kutoka PPRA walipofanya ziara ya kikazi Wilayani Same.

"Wakuu wote wa Idara na Vitengo hakikisheni kuwa manunuzi yote yanafanyika kwenye mfumo wa NesT kuanzia kutangaza zabuni"alisema.

Hata hivyo baadhi ya wakuu wa Idara walilalamikia mfumo kuwa taratibu na wakati mwingine kutopatikana kwa siku nzima.

Bw.Maregesi alisema changamoto zilizokuwepo kwenye mfumo zimeshafanyiwa kazi na sasa mfumo wa NesT hauna changamoto.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama alipokea maelekezo hayo na kuahidi kuendelea kuyatekeleza.

## WATUMISHI IDARA YA AFYA SAME WAPATIWA MAFUNZO YA GoTHOMIS



***Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same Dkt.Alex Alexander akimkabidhi Kompyuta mpakato (laptop) Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Same,Dkt .Devota Tumaini kama kitendea kazi muhimu kwenye majukumu yake.***

Serikali imewapatia mafunzo ya watumishi 94 wa Idara ya Afya juu ya matumizi ya mfumo wa usimamizi na uendeshaji  wa huduma za Afya hapa nchini (GoT-HoMIS) ili kuwawezesha kusimamia huduma hizo kwa weledi.

Akizungumzia mafunzo hayo Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same Dkt.Alex Alexander alisema mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa awamu kwa watumishi wa Afya ambapo hadi sasa zaidi ya Watumishi 130 wameshapata mafunzio hayo.

“Kwasasa taarifa zote za huduma zinazotolewa na idara ya afya zinatakiwa kuingizwa kwenye mfumo wa GoT-HoMIS na ndio maana tunaendelea kuwapatia mafunzo watumishi wa idara ya afya” alisema Dkt. Alex.

Wataalam waliopatiwa mafunzo hayo ni pamoja na timu ya usimamizi ngazi ya Wilaya (CHMT), Waganga Viongozi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wahasibu wa mapato Idara ya Afya, Wafamasia, Maafisa Afya na Wataalamu wa Maabara.

Wilaya ya Same ina Hospitali mbili na Viyuo vya Afya nane ambavyo vyote vimeshaunganishwa na Mfumo wa GoT-HoMIS na baadhi ya Zahanati.

“Tunatarajia hadi kumalizika mwaka huu wa fedha wa Serikali tutakua tumefikia Zahanati zote katika kuziunganisha na Mfumo wa GoT-HoMIS” alisema Dkt. Alex

## CCM YASHINDA 100% UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Same Mashariki na Same Magharibi Bw.Jimson Mhagama amesema tayari Viongozi wa Serikali za Vijiji 100 ambavyo vinaundwa na vitongoji 503 wameapishwa viapo vya uaminifu na kutunza siri pamoja na kiapo cha utii na uadilifu.

Bw.Mhagama amesema viongozi wote walioapishwa wanatokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), amesema zoezi la uapishaji limefanyika Novemba 28 kwenye vituo saba tofauti vya uapishaji ili kuwarahisishia viongozi hao kufika kwenye meneo hayo kirahisi.

“Tayari Wenyeviti wetu wa Vijiji,Vitongoji na wajumbe wa Halmashauri za vijiji wameapishwa ambapo idadi yao inafikia 2500, uapishwaji huu umekwenda sambamba na utoaji wa semina elekezi kwa viongozi hao”

Msimamizi huyo wa Uchaguzi alisema baada ya kuapishwa sasa viongozi hao wanaruhusiwa kisheria kuanza utekelezaji wa majukumu yao ya kuwatumikia wananchi katika masuala mbalimbali.

Akizungumza baada ya kuapishwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbakweni Kata ya Msindo Bw.Tuarira Mmbaga aliwashukuru wananchi wa kijiji chake kwa kumuamini na kumchagua.

“Nimefurahi kuapishwa leo, niwaahidi tu wananchi wa Mbakweni kwamba sasa tunakwenda kuanza kazi ya kuhakikisha kwamba kijiji chetu kinasonga mbele kwa maendeleo” alisema

## TFS WATAKIWA KUSAMBAZA MICHE YA MITI KWENYE TAASISI ZOTE



***Afisa wa Wakala wa Misitu (TFS) Yusuph Kajia akiotesha mti kwenye shule ya Msingi Kisima katika kumbukizi ya kifo cha baba wa Taifa Mwl Julius Kambarage Nyerere Oktoba 14.***

Kaimu Afisa Tawala wa Wilaya ya Same Bw.Sixbert Sarmett amewataka Wakala wa Misitu (TFS) Kanda ya Kaskazini kuhakikisha kuwa wanasambaza

miche ya miti kwenye Taasisi zote za Serikali na binafsi Wilayani humo ili kuendelea kutunza mazingira.

Alitoa wito huo kwenye zoezi la upandaji miti  kwenye shule ya msing Kisima ikiwa ni maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo cha baba wa Taifa Mw. Julius Kambarage Nyerere .

“Pamoja na kumkumbuka baba wa Taifa lakini huu pia ni mwendelezo wa kampeni maalum ya uoteshaji miti ili kuifanya Wilaya ya Same kuwa ya kijani” alisema Bw.Sarmett ambapo alisema mvua za vuli zilizoanza kunyesha ni lazima zitumike vizuri kutunza mazingira.

Akimwakilisha Mkuu wa Wilaya hiyo Mheshimiwa Kasilda Mgeni kwenye zoezi hilo Bw.Sarmett kwa kushirikiana na TFS na  wadau wa mazingira pamoja na wanafunzi walifanikiwa kuotesha miti 250.

“ Lengo la Wilaya ni kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka ambapo mwaka jana tulifanikiwa kupanda miti milioni 1.4 na mwaka huu tunatarajia tufikie lengo letu la kuotesha miti milioni 1.5” alisema na kuwapongeza TFS kwa kuwezesha upatikanaji wa miche ya kutosha.

Aidha Bw.Sarmett alizitaka mamlaka kuhakikisha kuwa hatua kazi zinachukuliwa kwa wale wote wanaoharibu mazingira kwa kukata miti hovyo na wanaochoma mkaa.

Akizungumza kwenye zoezi hilo Meneja wa TFS Kanda ya Kaskazini Bw. James Nshare alisema taasisi hiyo itaendelea kusambaza miche ya miti kwenye taasisi zote kama ilivyoelekezwa.

“Na watu binafsi pia wanaohitaji miche ya miti tunawakaribisha waje tutawapatia bure”Alisema Bw.Nshare.s

## CHANGIA ADA YA UZOAJI TAKA KUWEKA MJI SAFI

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



***Mkuu wa Wilaya ya Same mheshimiwa Kasilda Mgeni (kulia) akiwasaidia Mafundi kuchanganya zege kwaajili ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha Tano na Cha sita kwenye shule ya Sekondari Misufini-Goma.Mkuu wa Wilaya alifika shuleni hapo kukagua maendeleo ya ujenzi***



***Mkuu wa Wilaya ya Same mheshimiwa Kasilda Mgeni (kulia) akimkabidhi Kishwambi Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe,Yusto Mapande, Halmashauri ya Wilaya ya Same imewanunulia vishkwambia Madiwani 46 wa Halmashauri hiyo ili kuwawezesha kutekeleza vema majukumu yao.***




***Serikali imemkabidhi Trekta Mkulima Bora wa Pamba Wilayani Same Bw.Gabriel Mbwambo ambaye anatokea Kata ya Kisiwani.Piucha hii inamuonesha Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Kasilda Mgeni akimkabidhi Bw.Mbwambo hati ya Mkulima Bora na Trekta.***



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**


**S.L.P 138,SAME**

**Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Desemba 2024 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz  Same DC  samedc2022***